

Nia hamuoni rafiki  
yake. Kila wakati huwa  
anajificha. Nia anapata  
taabu kumtafuta. Nia  
anawaza... Oh! Nia  
amepata suluhisho.



Siku ya Jumatatu,  
alimpaka rangi  
nyekundu. Ili amuone  
kwa urahisi. "Uko  
wapi?" Nia  
anamtafuta.




"Niko kwenye matufaa  
mekundu."



Siku ya Jumanne  
alimpaka rangi ya  
chungwa ili amuone  
kwa urahisi.





Rafiki yake akajificha  
kwenye matunda.

Siku ya Jumatano nayo alimpaka  
rangi ya manjano. "Nikimpaka  
rangi hii nitamuona kwa urahisi." Nia aliwaza.






Tazama niko huku.

Siku ya Alhamisi, aliamua kumpaka  
rangi ya kijani.



Tazama rafiki yake Nia alikojificha.






Siku ya Ijumaa,  
alimpaka rangi ya  
samawati.




Rafiki alijificha kwenye  
picha iliyobandikwa  
ukutani.



Siku ya Jumamosi  
alimpaka yangi ya  
zambarau.



Alificha kwenye  
zabibu mbivu.



Siku ya Jumapili, Nia  
alipata suluhisho.  
Alimpaka rangi za  
upinde wa mvua.



Oh! Leo rafiki yake Nia  
hana tena pa kujificha.  
Anaonekana kwa  
urahisi.

